# Kushughulikia *unyanyasaji wa kifedha.*



## Unyanyasaji wa kifedha ni nini?

Unyanyasaji wa kifedha hutokea wakati pesa zinapotumiwa kama njia ya kupata nguvu na kudhibiti mtu mwingine. Unyanyasaji wa kifedha unaweza kuwanasa watu waliopo katika uhusiano dhalimu, na pia unaweza kuathiri uwezo wao wa kuishi salama wanapoamua kuondoka.

## Hali imeenea kwa kadri gani?

Nchini Australia, hadi 16% ya wanawake watapitia unyanyasaji wa kifedha katika maisha yao[1], na wanaume wanaweza kuathirika pia.

Unyanyasaji wa kifedha unaweza kuathiri watu kutoka asili mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kikabila na mielekeo yote ya kijinsia. Watu wenye ulemavu wana uwezekano mkubwa wa kuwa katika hatari kubwa ya kunyanyashwa kifedha kiuchumi na kifedha kutokana na sababu kama vile kuwategemea wengine, ukosefu wa ufikiaji wa rasilimali za kifedha, vikwazo vya kupata manufaa ya ustawi wa jamii na uzoefu mdogo katika kudhibiti fedha[2].

Ni kawaida kwa watu kuona haya na kulemewa wakati wa kuzungumza kuhusu unyanyasaji wa kifedha.

Ni muhimu kujifunza dalili za unyanyasaji wa kifedha, ni wapi pa kupata msaada, na jinsi ya kusaidia jamaa au rafiki ambaye anaweza kuwa katika hatari. Hii inaweza kusaidia waathiriwa kunusurika na kurejesha uhuru wao wa kifedha.

## Kutambua unyanyasaji wa kifedha

Licha ya kuenea kwake, unyanyasaji wa kifedha unaweza kuwa mgumu kuutambua:

- Wengi huona ni vigumu kutambua kwamba wako katika uhusiano ambao una unyanyasaji wa kifedha.
- Unyanyasaji wa kifedha unaweza kuanza kwa taratibu na kuendelea kwa muda.
- Katika tamaduni fulani, inaweza kuchukuliwa kama jambo linalokubalika kwa mtu mmoja kudhibiti fedha zote za familia.
- Wakati mwingine, pesa huonekana kama jambo la kibinafsi ambalo halijadiliwi waziwazi.

[1] Kutin, Russell, Reid (2017), Economic Abuse between intimate partners in Australia: prevalence, health status, disability and financial stress, Australian and New Zealand Journal of Public Health

[2] www.commbank.com.au/content/dam/commbank-assets/support/2021-09/unsw-disability-report-4.pdf

Commonwealth Bank of Australia ABN 48 123 123 124 AFSL na leseni ya mkopo ya Australia 234945.

## Baadhi ya Dalili za Unyanyasaji wa Kifedha:

Hauna uhakika ikiwa uko au hauko katika uhusiano wenye unyanyasaji wa kifedha?
Jiulize maswali yafuatayo:

Je, mpenzi wako amekuzuia kupata kazi au kwenda kufanya kazi?

Je, umewahi kushinikizwa na watu walio karibu na wewe ili uache kujipatia riziki au kutumia pesa zako mwenyewe?

Je, mpenzi wako hukataa kulipa fedha za malezi ya mtoto au kukusaidia kwa malezi ya watoto?

Je mpenzi wako hudhibiti jinsi pesa zote za familia zinavyotumika?

Je, mpenzi wako hufuatilia fedha unazotumia au hukuulizaumuonyeshe risiti zote za manunuzi?

Je, wewe hunyimwa fedha kila wakati au huhitaji kuomba pesa kwa ajili ya matumizi yako ya kimsingi au ya watoto wako?

Je, umewahi kuzuiliwa kuchangia katika kipato cha familia?

Je, umeulizwa kufanya kazi au 'fadhila' ili ulipwe fedha?

Je, umelazimishwa kuchukua mkopo au kadi ya mkopo kwa kutumia jina lako?

Je, mpenzi wako huweka fedha zake au fedha za familia kwa siri?

Je, maoni yako kuhusu maamuzi makubwa ya kifedha hupuuzwa?

Je, unalazimishwa kufanya kazi katika biashara ya familia bila kulipwa?

## Jinsi ya kupata msaada

Ikiwa wewe au mtu unayemjua anapitia unyanyasaji wa kifedha, au ikiwa huna uhakika, unaweza kupata huduma bila malipo. Ikiwa una hali ya dharura au hujisikii salama, piga simu kila wakati kwa **000**.

- Kama hatua ya kwanza ya mawasiliano tunakushauri upige simu kwa **1800RESPECT** kupitia **1800 737 732**. Hii ni huduma ya bila malipo na ya siri ambayo si sehemu ya Commonwealth Bank.
- Ikiwa unahitaji mkalimani au mtafsiri, unaweza kutumia Huduma ya simu ya Utafsiri na Ukalimani (TIS National) kwa **131 450**, taja lugha yako unayohitaji na uwaombe wapigie 1800RESPECT katika 1800 737 732. TIS National inapatikana bila malipo
- Vinginevyo, unaweza kupigia **1800RESPECT** katika **1800 737 732** na uombe mkalimani. Mshauri atafanya mipangilio.
- Ikiwa una wasiwasi kuhusu tabia, kuna usaidizi wa bila malipo na wa siri unaopatikana. Pigia Huduma ya Rufaa ya Wanaume **1300 766 491** au upige gumzo mtandaoni katika **ntv.org.au**.

Ili kupata maelezo zaidi kuhusu usaidizi, nenda kwenye **www.commbank.com.au/support/next-chapter.html**

Kwa mwongozo wa kina zaidi soma Mwongozo wa Utambuzi na Urejeshaji kwenye **tovuti ya CommBank**.